easytvet.com

Jina la Mtahiniwa: ______________________ Nambari: ______________/________

7015/2
LUGHA YA KISWAHILI
Aprili 2019
Saa: $1\frac{1}{2}$

Sahihi ya Mtahiniwa: ______________

Tarehe: ______________________

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# CERTIFICATE IN EARLY CHILDHOOD DEVELOPMENT AND EDUCATION

LUGHA YA KISWAHILI

**Saa $1\frac{1}{2}$**

**MAAGIZO**

*Andika nambari na jina lako kwenye nafasi ulizoachiwa.*
*Tia sahihi yako na tarehe kwenye nafasi ulizoachiwa.*
*Mtihani huu una sehemu tatu:* ***Insha*, *Ufahamu*** *na* ***Matumizi ya Lugha***.
*Andika majibu yako kwenye nafasi ulizoachiwa.*
*Usitoe karatasi yoyote katika kijitabu hiki.*
***Andika majibu yote kwa lugha ya Kiswahili***.

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| SEHEMU | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| I | 15 | |
| II | 15 | |
| III | 20 | |
| JUMLA | 50 | |

**Kijitabu hiki kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawa sawa na kuwa maswali yote yamo.**

© 2019 The Kenya National Examinations Council

easytvet.com

## SEHEMU YA KWANZA: INSHA (alama 15)

*Jibu swali la 1 au la 2.*

*Andika insha moja isiyopungua maneno 300 kuhusu mojawapo ya mada zifuatazo:*

1. Sekta ya kilimo imekumbwa na matatizo mengi. Thibitisha kauli hii.

2. Tunga kisa kinachodhihirisha ukweli wa: Haba na haba hujaza kibaba.

easytvet.com

## SEHEMU YA PILI: UFAHAMU (alama 15)

3. *Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.*

Binadamu tangu mwanzo amekuwa akishiriki katika michezo anuwai ambayo hutofautiana kulingana na umri; kuna michezo ya wazee, ya vijana na ya watoto wa viwango mbalimbali. Isitoshe, miongoni mwa watoto michezo ni tofauti ikizingatiwa viwango vyao katika maisha. Kwa mfano, kuna michezo ya watoto walio katika shule za upili, za msingi na za chekechea.

Shule za chekechea huhusisha watoto wenye umri usiozidi miaka mitano. Baadhi ya michezo yao ni kufungana macho na wenzao au na mwalimu kwa vijitambaa na kuulizwa kuwatafuta na hata kuwatambua wengine. Vile vile, watoto hawa hucheza michezo kama: mwajificho, kukimbia na kuruka kamba.

Umuhimu wa michezo ya watoto hauwezi kukadirika. Michezo huchangia katika kukuza maadili ya watoto. Maadili haya huweza kuwafaa hadi ukubwani. Kwa mfano, wanapohusishwa katika michezo, watoto huanza kukuza mahusiano mema miongoni mwao na wanajamii wengine. Watoto wanaocheza pamoja hufurahiana na kukuza upendo. Si ajabu kuona hata wengine wakifunga ndoa baadaye. Fauka ya hayo, umoja na ushirikiano hukuzwa kupitia michezo mbalimbali. Watoto wanapojigawa katika vikundi, wao hushindana na kujitambulisha kimakundi. Mathalan, wanaoshiriki katika kikundi kimoja hujiona kuwa kitu kimoja.

Vipawa navyo hukuzwa kupitia kwa michezo. Uwezo wa kuongoza huanza kukuzwa na kupaliliwa wakati mwalimu anapowahusisha wanafunzi kuwaongoza wenzao kwenye vikundi mbalimbali. Wengine husimamia vifaa vya kuchezea kama vile mipira, kamba na kata miongoni mwa vingine. Uongozi wa aina hii huwafunza watoto uwajibikaji. Pia, vipawa vya uanariadha hugunduliwa mapema wakati watoto wanapohusishwa katika michezo ya riadha wakiwa wadogo. Walimu huvigundua na kuvikuza vipawa hivi au kuwapendekezea wanaohusika kuviendeleza baadaye.

Mazoezi ya viungo vya mwili ni muhimu kwa watoto. Viungo hivi vinapofanyishwa mazoezi, huwafanya watoto kukua wakiwa wenye **siha** na kuepukana na baadhi ya maradhi kama vile shinikizo la damu. Aidha, mazoezi huwezesha akili kufanya kazi vizuri.

Ni jambo la kusikitisha kuwa jinsi hali ilivyo sasa katika shule za chekechekea ni tofauti na inavyopaswa kuwa. Siku hizi, watoto wa chekechea hushirikishwa katika masomo mengi mapema mno. Watoto hawa hubebeshwa marundo ya vitabu asubuhi na jioni. Vile vile, wao hupewa kazi nyingi za ziada ambazo wanatarajiwa kuzifanyia nyumbani, hawana muda wa kucheza. Licha ya hayo, wengine wao hulazimishwa na wazazi kupitia kwa ushawishi wa walimu kufanyiwa mafunzo ya ziada wakati wa likizo. Mambo haya huwadumaza watoto katika ukuaji wao.

easytvet.com

Ni muhimu kuwaacha watoto wakue kama watoto. Ni jukumu la wazazi, walimu na mashirika ya umma yanayowatetea watoto kuungana mikono. Wajitokeze kuvilaani vitendo vyovyote ambavyo vinawanyima watoto wadogo haki yao ya kucheza. Kucheza ni miongoni mwa haki za watoto ambazo zimeorodheshwa katika hati mbalimbali zinazohusu haki za watoto. Serikali yetu tukufu nayo isiachwe nyuma. Ifuatilie kwa makini utekelezaji wa haki za watoto nyanjani. Yeyote yule atakayepatikana akikiuka haki hizo **akione kilichomtoa kanga manyoya**.

(a) Kulingana na taarifa, taja kigezo kinachotumiwa kuainisha michezo. (alama 1)

---

(b) Tambua maadili **matatu** yanayotokana na michezo ya watoto kama yanavyojitokeza katika kifungu. (alama 3)

---

(c) Taja jinsi **mbili** ambazo walimu huchangia katika ukuaji wa vipawa vya watoto. (alama 2)

---

(d) Eleza faida **mbili** za mazoezi kwa watoto katika kifungu ulichokisoma. (alama 2)

---

easytvet.com

**SEHEMU YA PILI: UFAHAMU** (alama 15)

3. *Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.*

Binadamu tangu mwanzo amekuwa akishiriki katika michezo anuwai ambayo hutofautiana kulingana na umri; kuna michezo ya wazee, ya vijana na ya watoto wa viwango mbalimbali. Isitoshe, miongoni mwa watoto michezo ni tofauti ikizingatiwa viwango vyao katika maisha. Kwa mfano, kuna michezo ya watoto walio katika shule za upili, za msingi na za chekechea.

Shule za chekechea huhusisha watoto wenye umri usiozidi miaka mitano. Baadhi ya michezo yao ni kufungana macho na wenzao au na mwalimu kwa vijitambaa na kuulizwa kuwatafuta na hata kuwatambua wengine. Vile vile, watoto hawa hucheza michezo kama: mwajificho, kukimbia na kuruka kamba.

Umuhimu wa michezo ya watoto hauwezi kukadirika. Michezo huchangia katika kukuza maadili ya watoto. Maadili haya huweza kuwafaa hadi ukubwani. Kwa mfano, wanapohusishwa katika michezo, watoto huanza kukuza mahusiano mema miongoni mwao na wanajamii wengine. Watoto wanaocheza pamoja hufurahiana na kukuza upendo. Si ajabu kuona hata wengine wakifunga ndoa baadaye. Fauka ya hayo, umoja na ushirikiano hukuzwa kupitia michezo mbalimbali. Watoto wanapojigawa katika vikundi, wao hushindana na kujitambulisha kimakundi. Mathalan, wanaoshiriki katika kikundi kimoja hujiona kuwa kitu kimoja.

Vipawa navyo hukuzwa kupitia kwa michezo. Uwezo wa kuongoza huanza kukuzwa na kupaliliwa wakati mwalimu anapowahusisha wanafunzi kuwaongoza wenzao kwenye vikundi mbalimbali. Wengine husimamia vifaa vya kuchezea kama vile mipira, kamba na kata miongoni mwa vingine. Uongozi wa aina hii huwafunza watoto uwajibikaji. Pia, vipawa vya uanariadha hugunduliwa mapema wakati watoto wanapohusishwa katika michezo ya riadha wakiwa wadogo. Walimu huvigundua na kuvikuza vipawa hivi au kuwapendekezea wanaohusika kuviendeleza baadaye.

Mazoezi ya viungo vya mwili ni muhimu kwa watoto. Viungo hivi vinapofanyishwa mazoezi, huwafanya watoto kukua wakiwa wenye **siha** na kuepukana na baadhi ya maradhi kama vile shinikizo la damu. Aidha, mazoezi huwezesha akili kufanya kazi vizuri.

Ni jambo la kusikitisha kuwa jinsi hali ilivyo sasa katika shule za chekechekea ni tofauti na inavyopaswa kuwa. Siku hizi, watoto wa chekechea hushirikishwa katika masomo mengi mapema mno. Watoto hawa hubebeshwa marundo ya vitabu asubuhi na jioni. Vile vile, wao hupewa kazi nyingi za ziada ambazo wanatarajiwa kuzifanyia nyumbani, hawana muda wa kucheza. Licha ya hayo, wengine wao hulazimishwa na wazazi kupitia kwa ushawishi wa walimu kufanyiwa mafunzo ya ziada wakati wa likizo. Mambo haya huwadumaza watoto katika ukuaji wao.

easytvet.com

Ni muhimu kuwaacha watoto wakue kama watoto. Ni jukumu la wazazi, walimu na mashirika ya umma yanayowatetea watoto kuungana mikono. Wajitokeze kuvilaani vitendo vyovyote ambavyo vinawanyima watoto wadogo haki yao ya kucheza. Kucheza ni miongoni mwa haki za watoto ambazo zimeorodheshwa katika hati mbalimbali zinazohusu haki za watoto. Serikali yetu tukufu nayo isiachwe nyuma. Ifuatilie kwa makini utekelezaji wa haki za watoto nyanjani. Yeyote yule atakayepatikana akikiuka haki hizo **akione kilichomtoa kanga manyoya**.

(a) Kulingana na taarifa, taja kigezo kinachotumiwa kuainisha michezo. (alama 1)

(b) Tambua maadili **matatu** yanayotokana na michezo ya watoto kama yanavyojitokeza katika kifungu. (alama 3)

(c) Taja jinsi **mbili** ambazo walimu huchangia katika ukuaji wa vipawa vya watoto. (alama 2)

(d) Eleza faida **mbili** za mazoezi kwa watoto katika kifungu ulichokisoma. (alama 2)

easytvet.com

(e) Huku ukirejelea kifungu, andika matatizo **matatu** yanayowakumba watoto wa shule za chekechea. (alama 3)

(f) Kwa mujibu wa kifungu, bainisha wahusika **wawili** wanaotegemewa kusuluhisha matatizo ya watoto. (alama 2)

(g) Eleza maana ya: (alama 2)

(i) siha

(ii) akione kilichomtoa kanga manyoya

easytvet.com

## SEHEMU YA TATU: MATUMIZI YA LUGHA (alama 20)

*Jibu maswali **YOTE** katika sehemu hii.*

4. (a) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: (alama 2)

Kiwakilishi +Kitenzi

______________________________

______________________________

(b) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo. (alama 2)

Ufagio umenunuliwa leo.

______________________________

______________________________

(c) Kanusha sentensi ifuatayo: (alama 1)

Ukweli wa mambo utajulikana.

______________________________

______________________________

(d) Andika sentensi ifuatayo kwa wingi. (alama 2)

Mama amekwenda sokoni.

______________________________

______________________________

(e) Geuza sentensi ifuatayo iwe katika kauli ya kutendeka. (alama 2)

Amevaa rinda lake asubuhi.

______________________________

______________________________

(f) Taja neno moja moja linalopatikana katika ngeli ya: (alama 2)

(i) U - ZI ______________________________

(ii) A - WA kuku, ngombe ______________________________

easytvet.com

(g) Sahihisha sentensi ifuatayo: (alama 1)

Nilipofika kulinipendeza.

nilipendezwa

(h) Akifisha sentensi ifuatayo: (alama 3)

tembea taratibu mwalimu alimweleza

(i) Sehemu ya mguu kati ya goti na unyayo huitwa ______ (alama 1)

(j) Pambo hili huvaliwa wapi? (alama 1)

mkanda ______

(k) Rangi ya mbingu ni ______ (alama 1)

(l) Mtu ambaye ni maridadi huitwa ______ (alama 1)

(m) Kulikuwa na jamaa watatu. Wawili ni baba na wawili ni watoto. Hawa ni kina nani?

______ (alama 1)

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**